RISALA YA UTII YA WANANCHI WA WILAYA YA KIGAMBONI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MH. SAMIA SULUHU HASSAN KWENYE MBIO ZA MWENGE WA UHURU WA KITAIFA MWAKA 2022
WILAYA YA KIGAMBONI TAREHE 13/ 05/ 2022

2.0 UTANGULIZI

Mhe. Rais, Viongozi na Wananchi wa Wilaya ya Kigamboni tunayo furaha na heshima kubwa kuwakaribisha Vijana sita (6) shupavu wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2022, katika Wilaya yetu ya Kigamboni **'KARIBUNI SANA WILAYA YA KIGAMBONI'.**

3.0 UJUMBE WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2022

Mhe. Rais, Tumepokea Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 unaohusu Sensa ya Watu na Makazi chini ya kauli mbiu isemayo **"Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo: Shiriki kuhesabiwa, tuyafikie Maendeleo ya Taifa."**

Mhe. Rais, Sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi, hali ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi. Takwimu hizi za msingi ndiyo zinazoweza kuanisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum wakiwemo watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

Mhe. Rais, Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Wilaya ya Kigamboni ilikuwa na jumla ya watu **162,932** na kaya **40,133**. Kati ya hao wanaume walikuwa **81,199** na wanawake walikuwa **81,733.** Kwa mujibu wa ongezeko la watu la asilimia **5.6** kwa mwaka hadi kufikia mwaka **2019** Manispaa ya Kigamboni ilikisiwa kuwa na watu **238,591**. Kati yao wanaume ni **118,905** na wanawake ni **128,808**. Ongezeko hili limetokana na kukua kwa kasi kwa Manispaa ya Kigamboni.

Mhe. Rais, Kwa kutambua umuhimu wa Sensa ya watu na Makazi itakayofanyika mwezi Agosti, 2022, Manispaa ya Kigamboni imekwisha unda Kamati za Sensa ngazi ya Wilaya, Kata na Mitaa ambapo jumla ya Kamati **77** zimeundwa kama ifuatavyo: - Kamati ya Sensa ya Wilaya (**1**); Kamati za Sensa za Kata (**09**); Kamati za Sensa za Mitaa (**67**) na kupewa majukumu yake. Pia Manispaa imetenga fedha kiasi cha Tsh. **46,500,000.00** kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya maandalizi ya awali ya utoaji wa elimu na uhamasishaji juu ya umuhimu wa sensa.

Mhe. Rais, Aidha Manispaa imetekeleza maelekezo ya Serikali ya kuwa na Mfumo wa Kieletroniki wa Anwani za Makazi na Postikodi kwa ajili ya kupata taarifa zitakazotumika kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa kuwezesha kufanya ufuatiliaji na uhakiki wa maeneo na nyumba ambazo zimehesabiwa. Halmashauri imefanikiwa kutoa mafunzo ya Mfumo wa NaPA kwa vijana **183** waliofanya zoezi hili pamoja na anwani za makazi kwa viongozi **177.** Pia, Makadirio ya nyumba na viwanja yaliyofanyika ni nyumba **49,353** na zilizoingizwa katika mfumo ni nyumba **58,508** sawa na asilimia **118.5** Aidha, makadirio ya barabara/mitaa yalikuwa **1,864** na zilizoingizwa katika mfumo ni **3,617.**

Mhe. Rais, Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi katika Manispaa ya Kigamboni zimekuwa chachu kubwa ya mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo: -

3.1 Sekta ya Elimu.

Mhe. Rais, Kuwepo kwa takwimu hizi kumesaidia shule zote za Serikali (Msingi **34** na Sekondari **15**) kuweza kupanga mipango ya uboreshaji wa miundombinu inayohitajika, kuwezesha utoaji wa Elimu bure kwa sababu ya kuwepo kwa takwimu ambazo zimesaidia utoaji chakula na hata kuwezesha kufahamika kwa gharama za mitihani na hivyo kusaidia kupandisha kiwango cha ufaulu. Kupitia takwimu hizo jumla ya mabweni **2** ya watoto wenye mahitaji maalum yanajengwa katika shule ya Msingi Chekeni Mwasonga (bweni 1 la fedha za UVIKO – 19 na lingine TEA), Vyumba vya madarasa **38** vimejengwa kupitia fedha za UVIKO - 19, vyumba vya madarasa **23** vimejengwa na vingine **17** vinaendelea kujengwa kupitia fedha za mapato ya ndani.

3.2 Sekta ya Afya:

Mhe. Rais, Matumizi ya takwimu hizi yamesaidia uendeshaji wa vituo vyote **22** vinavyotoa huduma za afya katika wilaya yetu, ikiwemo upatikanaji wa dawa za kutosha kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma, kuwezesha uboreshaji wa miundumbinu ya afya, ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 kuna vituo vya afya **3** na jengo **1** la wagonjwa wa kifua kikuu vinaendelea kujengwa kupitia fedha za Tozo ya miamala ya simu na fedha kutoka Serikali Kuu. Sambamba na haya upangaji wa Mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika sekta ya afya umetumia takwimu hizi ili kujua hasa namna bora ya kuweza kuboresha huduma zote za afya kwa ustawi wa jamii, zikiwemo takwimu za utoaji wa huduma za lishe bora kwa watoto na jamii.

3.3 Sekta ya Barabara:

Mhe. Rais, Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini – TARURA hutumia takwimu hizi ili kuweza kupanga vipaumbele katika utekelezaji wa bajeti za ujenzi wa barabara. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya km **0.65** za barabara zinaendelea kujengwa kwa kutumia fedha za Tozo na za Mfuko wa barabara. Kati ya hizo km **0.30** zimekamilika na km **0.35** za fedha za Tozo inaendelea kujengwa.

3.4 Sekta ya Maji:

Mhe. Rais, Wakala wa Maji Mijini na Usafi wa Mazingira (DAWASA) hutumia takwimu hizi katika kuandaa mipango na utekelezaji wa uchimbaji wa visima virefu na vifupi pamoja na ujengaji wa matanki pamoja na usambazaji wa maji katika maeneo ya wilaya yetu.

3.5 Sekta ya maendeleo ya jamii:

Mheshimiwa Rais, Halmashauri kupitia takwimu hizi imeendelea kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutenga asilimia **10** ya mapato ya ndani ili kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wananchi kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipanga kutoa mikopo ya kiasi cha Tsh. **467,140,632.09** ambayo ni asilimia **10** ya mapato ya ndani. Hadi kufikia Machi 2022 Manispaa imetoa jumla ya T.sh **472,282,150.00** kwa vikundi **49** (wanawake **27**, vijana **16** na watu wenye ulemavu **6**). Aidha, mikopo mingine imeendelea kutolewa kupitia marejesho yanayofanyika.

3.6 Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri:

Mhe. Rais, Kupitia takwimu hizi Halmashauri imeweza kufahamu maeneo ya kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato kutokana mzunguko mkubwa wa kibiashara unaotokana na kuangalia wingi wa wakazi wa maeneo hayo, hivyo kuweza kufunga Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (LGRCIS) na mashine za kukusanyia mapato za PoS,

ambazo zimeongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka Tsh. **3,432,340,089.00** mwaka 2016/2017 kabla ya mfumo hadi Tsh. **8,487,415,365.56** kwa mwaka 2020/2021 na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia tarehe 31, Machi Halmashauri imekusanya jumla Tsh. **5,352,259,476.59** sawa na asilimia 76 ya makisio ya mapato ya mwaka 2021/2022.

3.7 Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao:

Mhe. Rais, Jeshi la Polisi hutumia takwimu hizi katika kupanga mipango ya ulinzi na usalama wa Raia na mali zao. Kwa kutumia takwimu hizi Wilaya inajenga kituo kikubwa cha polisi kimoja **(1)** kilichopo Gezauloloe kata ya Somangila kwa ajili ya kuongeza ulinzi kwa Raia na mali zao hivyo kusaidia kuendelea kwa shughuli za kiuchumi na maendeleo kwa wakazi wa maeneo yote ndani ya Wilaya.

4.0 TAARIFA ZA FEDHA ZA TOZO

Mhe.Rais, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa imepokea fedha za tozo za simu kiasi cha Tsh. **250,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha afya Kichangani li kuwezesha ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) na Jengo la Maabara. Utekelezaji kwa jengo la OPD umefikia hatua ya Upauaji, kwa maana ya uwekaji wa kenchi na maandalizi kwa ajili ya uezekaji yanaendelea. Kwa jengo la Maabara utekelezaji wa upandishaji wa tofali juu ya lenta umekamilika na maandalizi kwa ajili ya upauaji yanaendelea. Fedha zilizotumika hadi sasa ni jumla Tsh. **131,709,636.74**.

5.0 TAARIFA YA FEDHA ZA UVIKO 19

Mhe. Rais, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipangiwa kupokea Tsh. **1,260,000,000.00** kati ya fedha hizo Tsh. **420,000,000.00** ni za mashine ya x-ray, Tsh. **80,000,000.00** ni za ujenzi wa madarasa **4** katika vituo shikizi, Tsh. **80,000,000.00** ni za ujenzi wa bweni **1** la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum na Tsh. **680,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **34** ya shule za sekondari pamoja na ununuzi meza na viti **1700** na madawati **100**. Hadi kufikia sasa Ujenzi wa madarasa yote **38** umekamilika na madarasa yanatumika. Ujenzi wa bweni **1** la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum unaendelea na umefikia hatua ya umaliziaji, kazi zinazoendelea ni upigaji wa rangi na ufungaji wa gypsum na fedha zilizotumika hadi sasa ni Tsh. **80,000,000.00** na ununuzi wa mashine ya X-ray utanunuliwa kwa Halmashauri zote kupitia TAMISEMI.

6.0 UKAMILISHAJI NA UENDELEVU WA MIRADI ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE MWAKA 2019

Mhe. Rais, Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2019 ulipitia jumla ya miradi mitano (**5)** katika kata nne (**4)** (Vijibweni, Kibada, Mjimwema na Somangila), katika sekta ya Afya miwili (**2)**, Elimu Msingi mmoja (**1)**, Viwanda kimoja (**1**) (Kiwanda cha Vifungashio) na Sekta ya Maji mmoja (**1)**. Aidha miradi mitatu (**3**) ilizinduliwa ambayo ni madarasa mawili (**2**) katika shule ya Msingi Vijibweni, uzinduzi wa kiwanda cha Vifungashio na uzinduzi wa jengo la mionzi (X-Rays) katika Hospitali ya Vijibweni na miradi miwili(**2**) ilikaguliwa ambayo ni ujenzi wa chuo cha afya Kigamboni na ukarabati wa mradi wa maji Gezaulole.

Mhe. Rais, miradi yote hii imekamilika na inaendelea kutoa huduma hadi sasa. Miradi yote mitano (**5)** iligharimu jumla ya Tsh. **13,814,718,625.33** ambapo Serikali Kuu ilichangia Tsh. **194,071,460.00**, Halmashauri Tsh. **262,647,165.33** na Wafadhili Tsh. **13,358,000,000.00.**

7.0 UKAMILISHAJI NA UENDELEVU WA MIRADI ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021

Mhe. Rais, Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Kigamboni ilikimbizwa kilometa **82.3** katika Tarafa tatu (**3**) (Kigamboni, Somangila na Pembamnazi) na Kata tano (**5**) (Vijibweni, Kigamboni, Mjimwema, Somangila na Kimbiji) na ulipitia miradi ya maendeleo ya ujenzi mitano (**5**) katika Sekta za Afya miradi miwili (Uwekaji mawe ya msingi katika miradi ya ujenzi wa Zahanati na Jengo la Mionzi katika Kituo cha afya Kimbiji), ambayo miradi hii yote bado haijakamilika ila itakamilika na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2022/2023. Elimu miradi miwili (Uzinduzi wa Jengo la Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Elimu), ambalo linatumika na Uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa Bweni la Wanawake shule ya Sekondari Kimbiji), ambalo bado halijaanza kutumika ila litakamilika katika mwaka wa fedha 2021/2022, mradi mmoja (**1**) wa barabara (Ujenzi wa Barabara ya Azimio – Mashujaa yenye urefu wa kilomita **1.46**) ambayo imekamilika na mradi wa kikundi cha VEMA.

Mhe. Rais, Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 ina thamani ya Tsh. **1,306,469,431.75** zikiwemo Tsh. **31,110,000.00** za michango na nguvu za wananchi, Tsh. **113,226,829.64** za Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Tsh. **1,162,132,602.11** fedha toka Serikali Kuu.

8.0 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2022

Mhe. Rais, Mwenge wa Uhuru 2022 Manispaa ya Kigamboni umekimbizwa kilometa 103 katika Tarafa tatu (**3)** (Kigamboni, Somangila na Pembamnazi) na Kata saba (**7**) (Vijibweni, Kigamboni, Kibada, Kisarawe II, Pembamnazi, Somangila na Mjimwema) na umepitia miradi ya maendeleo ya ujenzi minne (**4**) katika Sekta za Afya miradi miwili (**2**) (Uwekaji mawe ya msingi katika mradi wa ujenzi Kituo cha afya Tundwi Songani na Kichangani), Elimu mradi mmoja (**1**) (Uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum shule ya Msingi chekeni Mwasonga), Barabara mradi mmoja (**1**) (Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Barabara ya Mikadi Beach – Shelaton). Pia mwenge ulipitia kukagua shughuli za kikundi cha vijana cha TAMU Milk kinachojishughulisha na usindikaji wa maziwa pamoja kikundi cha wanawake TUINUANE GROUP kinachojishughulisha na shughuli za uzoaji katika kata ya Vijibweni.**Mhe. Rais,** Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ina thamani ya Tsh. **1,469,720,959.42** zikiwemo Tsh. **54,000,000.00** za michango na nguvu za wananchi, Tsh. **129,758,249.42** za Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Tsh. **1,285,962,710.00** fedha toka Serikali Kuu. Aidha kwenye uwanja wa mkesha Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2022 umekagua mabanda mbalimbali ya shughuli za Kiuchumi na Kijamii ikiwemo mabanda ya mapambano dhidi ya dawa za Kulevya, mapambano dhidi ya Malaria, TAKUKURU, Vikundi vya Kiuchumi, Mfuko wa Afya ya Jamii, masuala ya Lishe, mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI na maandalizi ya sensa ya watu na makazi.

9.0 KIASI CHA FEDHA KILICHOCHANGWA KWA AJILI YA SHUGHULI ZA MBIO ZA MWENGE UHURU MWAKA 2022

Mhe. Rais, Hadi kufikia tarehe 12/05/2022, jumla ya Tsh. **54,000,000.00** taslimu zimechangwa kwa ajili ya shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ambapo Wadau wamechangia Tsh. **18,000,000.00** na Manispaa ya Kigamboni Tsh. **36,000,000.00**.

10.0 UTEKELEZAJI WA UJUMBE WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2022.

10.1 MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa VVU/UKIMWI chini ya kauli mbiu isemayo:- ***"Zingatia USAWA; Tokomeza UKIMWI na magonjwa ya Mlipuko"*** Hali ya maambukizi katika Wilaya ya Kigamboni imepungua kutoka 6.0% mwaka 2016 hadi 4.0% mwaka 2022. Elimu ya

kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI inatolewa katika Vituo vyote 41 vya huduma za afya kila siku.

Mhe. Rais, Katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya ikiwemo Hospitali ya Wilaya, vituo vya Afya na Zahanati kuna vitendanishi vya upimaji vya kutosha. Pia vituo vina dawa za kufubaza Virusi vya Ukimwi (VVU). Wagonjwa wenye mahitaji maalum wanafikishiwa dawa katika maeneo yao na wataalam wa huduma za VVU majumbani ambapo jumla ya watu **34,173 (me 11,377, ke 24,108)** wanapata huduma.

Mhe. Rais, Kwa mwaka 2021/2022 mama wajawazito wapatao **121** walikutwa na maambukizi kati ya kina mama wajawazito **10,521** waliopimwa virusi vya UKIMWI sawa na asilimia **1.4**. Aidha wakina mama hawa wote wamepatiwa ushauri nasaha na kuanzishiwa tiba ili kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, watoto **2** kati ya **232** waliozaliwa na wamama wenye VVU sawa na **0.8%** walikutwa na Maambukizi ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto.Wilaya inashirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo mashirika ya **MDH, FHI 360, MUKIKUTE, WASO, TAYOHUG, KIPENET na KIYODEN** katika kutekeleza afua mbalimbali za kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI.

10.2 MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa Malaria chini ya kauli mbiu isemayo:- ***"Ziro Malaria inaanza na Mimi- Nachukua hatua kuitokomeza"*****.** Manispaa imeweza kupunguza maambukizi ya malaria kutoka wagonjwa **12,029** mwaka **2019** sawa na **5.5%** ya watu **216,611** waliopima mpaka wagonjwa **10,251** mwaka **2021** sawa na **3.1%** ya watu **329,999** waliopima na hadi kufikia Machi, **2021** hakuna kifo chochote kilichosababishwa na malaria.

Mhe Rais Wilaya ya Kigamboni inatekeleza afua mbalimbali za kumkinga mama mjamzito asipate maambukizi ya Malaria. Afua hizo ni kutoa kinga ya vidonge vya SP kwa wajawazito pamoja na kugawa vyandarua vyenye viuatilifu kwa akina mama wajawazito. Jumla ya vyandarua **8,766** kati ya **10,391** sawa na asilimia **84.3** vimegawiwa kwa mama wajawazito na pia watoto chini ya umri wa miaka mitano **(5)** walipewa vyandarua **5,479** sawa na asilimia **82.7** ya watoto **8,748** waliohudhuria Kliniki.

10.3 MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Mhe Rais, Tumeupokea ujumbe wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya chini ya kauli mbiu isemayo:- **"Tuelemishane juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya, Kuokoa maisha".** Manispaa ya inaendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya pamoja na huduma ya ushauri nasaha. Wilaya ina nyumba 10 za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya ambazo zinamilikiwa na Watu binafsi, chini ya mwongozo wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya Tanzania.

Mhe. Rais, Wilaya kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama inaendelea na mapambano dhidi ya matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Machi 2022 matukio yalikuwa kama ifuatavyo: Bangi kesi **3**, kilo **5** na gramu **478** jumla ya Watuhumiwa **43**, kesi zilizofikishwa Mahakamani ni **22**. Mirungi kesi **1,** kilo **4** na gramu **76** Watuhumiwa **2**, Idadi ya kesi zilizofikishwa mahakamani **23** na kesi **8** zipo chini ya upelelezi kukamilisha taratibu za kupelekwa Mahakamani.

Mhe. Rais, Elimu inayohusiana na madhara ya dawa za kulevya imekuwa ikitolewa katika maeneo ya Mashuleni, minadani, kwenye vituo vya daladala na bodaboda, kwenye maeneo ya Wavuvi na ndani ya vituo vyote vya Afya. Pia, Wilaya imejenga Kituo cha kutoa huduma za madawa ya kulevya katika Hospitali ya Vijibweni kwa kuhudumia watu wa jinsia zote na

kuzingatia miundombinu kwa watu wenye ulemavu. Pia katika Wilaya kuna Asasi za **TAYOHAG, TEWWY** na **MKIKUTE** ambazo zinaendelea kutoa elimu inayohusiana na dawa za kulevya.

10.4 MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Mhe Rais, Tumeupokea ujumbe wa Rushwa chini ya kauli mbiu isemayo:- "**Kuzuia Rushwa ni Jukumu langu".** Kwa kutambua umuhimu wa kuzuia na kupambana na vitendo vya Rushwa kwa mwaka 2021/2022 Wilaya ya Kigamboni ilipokea malalamiko **65** kutoka Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, watumishi na watu binafsi na hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 uchunguzi wa malalamiko **22** unaendelea kufanyika. Majalada 04 yameombewa kibali cha mashtaka kwa RPO. Kesi **03** zinaendelea mahakamani na kesi 01 imeamuliwa na Mahakamani na mshitakiwa kuachiwa huru.

Mhe. Rais, Ili kuhakikisha panakuwepo na miradi endelevu ndani ya Wilaya, TAKUKURU imefanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa ili kuona inaendana na thamani halisi ya fedha zilizotolewa. Jumla ya miradi **44** ilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwemo miradi iliyotekelezwa kwa fedha za UVIKO -19.

10.5 LISHE BORA KWA AFYA IMARA

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa lishe bora kwa afya imara wenye kauli mbiu isemayo:- **"Lishe Bora ni Msingi wa Uchumi Imara".** Wilaya ya Kigamboni ina asilimia **0.2** ya watoto chini ya miaka mitano wenye utapiamlo mkali na asilimia **3.5** ya wanawake wajawazito wana upungufu wa damu. Manispaa imetoa mafunzo kwa watoa huduma wa afya **67** katika ngazi ya jamii na wamewasaidia wananchi kuelewa dalili za utapiamlo, jinsi ya kujiepusha na utapiamlo na namna bora za kupata huduma ya afya.

Mhe. Rais, Utapiamlo mkali umeshuka kutoka asilimia **0.4** kwa mwaka 2020/2021 mpaka **0.2** kwa mwaka 2021/2022. Pia Watoto waliopatiwa matone ya vitamini A ni **26,766** kati ya **28,175** waliotarajiwa ambao ni sawa na asilimia **95**.

10.6 HITIMISHO

Mhe. Rais, Pamoja na shukrani zetu kubwa kwako sisi Wananchi wa Wilaya ya Kigamboni tunatekeleza kwa vitendo ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wenye kaulimbiu **"Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo: Shiriki kuhesabiwa tuyafikie Maendeleo ya Taifa"**. Mwisho kwa niaba ya Uongozi wa Wilaya tunawatakia Vijana wote wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka, 2022 heri na baraka katika kufanikisha jukumu hili kubwa walilokabidhiwa na Taifa letu.

Mhe. Rais, Risala hii pia imeambatishwa na viambata **'A – T'** vinavyohusu taarifa za miradi na shughuli zilizopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022.

Naomba kuwasilisha.

MWENGE WA UHURU OYEEE!!!!

Fatma Almas Nyangasa
MKUU WA WILAYA
KIGAMBONI